# TANGAZO

## IJUE TOVUTI YETU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

Watumishi na Wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mnatangaziwa kuwa Tovuti ya Halmashauri yetu iko hewani na ilizinduliwa rasmi Tarehe: 27 / 03 / 2017.

### MALENGO YA KUANZISHA TOVUTI:

- Kukuwezesha kuijua Halmashauri yako zaidi ikiwemo historia yake pamoja na huduma zote zitolewazo kwa wananchi.
- Kukueleza miradi inayoendeshwa, bajeti (mapato na matumizi) na matukio mbalimbali.
- Kukuelimisha kuhusu sera, sheria, kanuni, taratibu, n.k.
- Kukupunguzia usumbufu na gharama za kufuata baadhi ya huduma katika ofisi za halmashauri hasa kwa kukueleza jinsi huduma fulani unavyoweza kuipata.
- Inaonyesha matangazo ya kazi mbalimbali, matangazo ya zabuni na Biashara.
- Pia unaweza kuona Maswali ya mara kwa mara (MMM) yanayoulizwa na wananchi kuhusu upatikanaji wa huduma zetu pamoja na majibu yake.

• Unaweza kuona orodha ya waheshimiwa madiwani pamoja na mawasiliano yao.

• Watumishi na Wananchi utakuta eneo la juu la rangi ya kijani lililoandikwa ***Malalamiko*** **Bofya** hapo ili uweze kuandika malalamiko yako na kututumia ili tuweze kuyashughulikia na taarifa nyingine nyingi utakutana nazo kwenye tovuti yetu.

## NAMNA YA KUINGIA KWENYE TOVUTI YETU

**Kwa kutumia kompyuta au simu ya kiganjani:**

• Unganisha mtandao kwenye kompyuta au simu yako,

• Fungua 'browser' yako mfano: **google crome, Mozilla, Safari, Opera n.k**

• Andika hivi: http://www.igungadc.go.tz

- Matangazo ya Biashara yanakaribishwa kwa walionayo ila yatalipiwa.

- Tembelea tovuti http://www.igungadc.go.tz utapata taarifa mbalimbali zinazoihusu ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

• Harafu bonyeza '**Enter**'.

Hapo ndipo utaweza kufungua tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwa mwonekano ufuatao:-





Edit FrequentAskedQue × | Home | Igunga District C × | Home | Urambo District × | 5a83f686c110d2082279 ×

igungadc.go.tz

## Habari Mpya
Zaidi

Mhe.Naibu Waziri Aongea na Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya Igunga

**Posted On: February 20th, 2018**

Mheshimiwa George Joseph Kakunda Naibu Waziri Ofisi ya Rais na Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa OR-Tamisemi, akiwa kwenye ziara ya kukagua shughuli za miradi ya maendeleo Wila...

Taratibu za Uhawilishaji Fedha TASAF III
**Posted On: February 16th, 2018**

Uzinduzi Utambuzi na upigaji Chapa Ng'ombe Wilaya ya Igunga
**Posted On: December 3rd, 2017**

Harambee Shule ya Sekondari Choma
**Posted On: December 2nd, 2017**

## Matukio
Zaidi

No records found

## Matangazo
Zaidi

1. Siku ya Usafi
   **-March 22, 2017**
2. Mkutano wa Baraza La Madiwani kufanyika tarehe 28, Aprili 2017
   **-March 27, 2017**
3. Kushiriki mazoezi ya pamoja kila Jumamosi ya pili ya mwezi
   **-March 26, 2017**

## Matangazo ya Kibiashara
Zaidi

No records found

## Zabuni
Zaidi

| Jina la Zabuni | Tarehe Iliyoongezwa | Tarehe ya Kumalizika |
|---|---|---|

## Ramani

## Dashibodi
- Taarifa za mapato (LGRCiS)
- Takwimu za sekta ya elimu
- Taarifa za shule (SIS)
- Taarifa za huduma za maji
- Taarifa za huduma za afya
- Taarifa za huduma ya elimu

Dashibodi Zaidi

## Takwimu za haraka
- Idadi ya Watu = 399727




**KARIBUNI SANA**
**TUIJENGE IGUNGA YETU.**

**Imetolewa na:**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Igunga
S.L.P 19
**IGUNGA.**

Barua pepe: igungadc@gmail.com
Tovuti: http://www.igungadc.go.tz

**Machi 2018.**